



BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI

TAARIFA KWA UMMA

USAJILI WA MITIHANI YA 26 YA BODI

Dodoma 17 Januari, 2023

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, mitihani ya 26 ya Bodi inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **16/05/2023** mpaka tarehe **19/05/2023**. Watahiniwa wote wanaelekezwa kufanya usajili kwa kupitia mfumo wa usajili wa Bodi wa <https://registration.psptb.go.tz> na pia kuhudhuria madarasa ya mafunzo kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo.

Mitihani hii itafanyika katika vituo vya **Dar es Salaam, Moshi, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Zanzibar**. Mwisho wa kupokea maombi ya kufanya mitihani hiyo ni tarehe **21/04/2023**.

WAOMBAJI WENYE SIFA KWA AJILI YA MITIHANI YA MEI, 2023:

- (1) Wahitimu wote waliomaliza vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za shahada, stashahada na astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2022 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya PSPTB.
- (2) Wadau wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi wasiokuwa na cheti cha CPSP.
- (3) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya Ununuzi na Ugavi kwa ngazi za stashahada, shahada au sifa za kitaaluma kutoka Bodi ya taaluma husika.

NB:

Watahiniwa wanaorudia baadhi ya mitihani kwa zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha masomo ya ngazi mbili zinazofuatana kwa masomo kuanzia mawili hadi Sita tu.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia **examinations@psptb.go.tz**

Imetolewa na:

S. A. Mdee

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI